
MUUNGANO WA VIONGOZI
WA AFRIKA KATIKA UDHIBITI
WA MALARIA

ALMA

# ALMA 2024 – MUHTASARI WA TAARIFA - ROBO YA PILI

## Utangulizi: Malaria - Kurejea kwa Dhoruba

Kutokomeza Malaria kunakabiliwa na dhoruba kamili, mjumuisho wa vitisho vingi ambavyo vinavuruga utekelezaji wa afua muhimu za kuokoa maisha kutokana na Malaria.





Mipango ya Malaria inabidi kila mara kukabiliana na changamoto mpya, kushindwa kutekeleza, teknolojia mpya na vikwazo vya rasilimali.

## Kufadhili Dhoruba: Upungufu Mkubwa

Kutokomeza Malaria kunakabiliwa na upungufu mkubwa wa kifedha. Kufikia mwaka 2026, dola za marekani bilioni 1.5 zinahitajika ili kudumisha utekelezaji wa afua zilizopo za Malaria ambazo tayari hazitoshi kuafikiwa kikamilifu. Upungufu huu unaohusishwa na msukosuko wa kifedha unaoendelea duniani, ambao unaweza kuwaacha zaidi ya watu milioni 400 bila ulinzi, kutokana na upungufu wa vyandarua vya muda mrefu zaidi ya milioni 200. Pia kuna mapungufu makubwa ya ufadhili katika utekelezaji wa Mipango Mikakati ya Kitaifa.


**Makadirio ya Ufadhiliwa wa Vyandarua - (2024-2026)**




Lengo limefikiwa / utekelezaji unaendelea
Juhudi zaidi zinahitajika kufikia lengo
Utekelezaji upo nje ya lengo
Hamna Takwimu/ Haihusiki

**Chanzo: Robo ya 2, 2024 Kadi ya Alama ya thamnini na Uwajibikaji ya ALMA**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka yake ya nchi yeyote.*

**% ya Mipango Mikakati ya Kitaifa iliyopata Ufadhili (2024-2026)**




Lengo limefikiwa / utekelezaji unaendelea
Juhudi zaidi zinahitajika kufikia lengo
Utekelezaji upo nje ya lengo
Hamna Takwimu/ Haihusiki

**Chanzo: Robo ya 2, 2024 Kadi ya Alama ya thamnini na Uwajibikaji ya ALMA**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka yake ya nchi yeyote.*

NCHI WANACHAMA
Algeria
Angola
Benin
Botswana
Burkina Faso
Burundi
Cameroon
Central African Republic
Cabo Verde
Chad
Comoros
Republic of Congo
Côte d'Ivoire
Democratic Republic of Congo
Djibouti
Egypt
Equatorial Guinea
Eritrea
Eswatini
Ethiopia
Gabon
Ghana
Guinea
Guinea Bissau
Kenya
Lesotho
Liberia
Libya
Madagascar
Malawi
Mali
Mauritania
Mauritius
Mozambique
Morocco
Namibia
Niger
Nigeria
Rwanda
Sahrawi Arab Democratic Republic
São Tomé and Príncipe
Senegal
Seychelles
Sierra Leone
Somalia
South Africa
South Sudan
Sudan
The Gambia
Togo
Tunisia
Uganda
United Republic of Tanzania
Zambia
Zimbabwe

Makadirio ya Mradi wa Malaria Atlas yanatabiri kwamba kama rasilimali zitaendelea kupungua kuanzia mwaka 2027 hadi 2029 **kutakuwa na wagonjwa milioni 112 wa ziada na vifo 280,700 ziada vitokanavyo na Malaria.** Tutaona ongezeko na milipuko ya ugonjwa wa Malaria barani Afrika. Ushahidi wa kihistoria unaonesha kuwa ugonjwa wa Malaria huongezeka haraka wakati ufadhili unakatwa, na programu kuondolewa na mapungufu ya ufadhili ndio yanatajwa kuwa ni sababu kuu ya kuibuka tena kwa Malaria.[1]


## Jinamizi linalokuja!

Takwimu kutoka kwa Mradi wa Malaria Atlas, unaochunguza hatari ya kupokea Malaria barani Afrika, inakadiria kuwa **kutokuwepo kabisa kwa udhibiti wa Malaria mwaka 2022 kungesababisha wagonjwa 558,275,474 na vifo milioni 2.8 vinavyotokana na Malaria**.[2] Hii inaonesha sio tu kuwa mafanikio ambayo tumeyapata yako hatarini lakini, ikiwa programu za kudhibiti Malaria hazitaendelezwa, tunaweza kuishia mahali pabaya zaidi kuliko tulivyokuwa miongo miwili iliyopita.

Athari ya mabadiliko ya tabia nchi hasa kuongezeka kwa mafuriko, vimbunga, na matukio mengine mabaya ya hali ya hewa yanazidisha hali hiyo, na kuandaa mazingira ya kuzuka tena kwa ugonjwa wa Malaria. Hii sio tu inatishia kuongezeka maambukizi ya Malaria lakini pia, huongeza mzigo wa magonjwa mengine yanayoenezwa na wadudu.

Aidha, Afrika inakabiliwa na ongezeko la vitisho vya kibailojia: usugu wa viuatilifu, usugu wa dawa za Malaria, pamoja na vimelea vya Malaria vinavyokwepa vipimo vya uchunguzi wa vipimo vya haraka na uvamizi wa mbu wapya wanaotishia maambukizi ya Malaria maeneo ya Mjini. Kwa bahati nzuri, tuna zana bora ambazo zinaweza kushughulikia vitisho hivi, lakini ni ghali zaidi. Vyandarua vipya vina athari kubwa katika kupunguza Malaria na vinaendelea kusambazwa kote barani Afrika; lakini matokeo bado hayajafikiwa kukilingana na matarajio. Zana zingine mpya pia zimeanza kutumika, kama vile chanjo ya Malaria ambayo lazima itumike pamoja na zana zingine zilizopo.


**Viuatilifu na Uwepo wa Usugu kwa mbu uliothibitishwa tangu mwaka 2010**




**Chanzo: Robo ya 2, 2024 Kadi ya Alama ya thamnini na Uwajibikaji ya ALMA**

*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka yake ya nchi yeyote.*

**% ya udhibiti wa wadudu waenezao magonjwa kwa mwaka jana na nyenzo mpya za vyandarua**




**Chanzo: Robo ya 2, 2024 Kadi ya Alama ya thamnini na Uwajibikaji ya ALMA**

*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka yake ya nchi yeyote.*

**Dharura za Kibinadamu na za Kiafya.** Kati ya mwaka 2019 na mwaka 2022, nchi 41 zenye ugonjwa wa Malaria zilikumbwa na majanga kama haya; Nyingi ya nchi hizi ziliona ongezeko kubwa la visa na vifo vya Malaria, na nchi chache zilipata janga la Malaria.[3]

**Mifumo Endelevu ya Afya – Dhidi ya kukuza upya kwa Malaria.**
**Uwekezaji wa Malaria ni uwekezaji katika kuimarisha mfumo na usalama wa Afya.**
Mipango ya Malaria iliyotoa mafunzo kwa wahudumu wa afya ya jamii ndani ya mifumo thabiti ya afya ya jamii; zinahitaji takwimu na ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa genomic**;** Zinahitaji uwezo wa kufanya makisio na usambazaji wa bidhaa; zinahitaji uwezo, na ufanisi katika kiwango cha uchunguzi; - vyote hivyo ni vipengele muhimu vya mifumo thabiti ya afya ikijumuisha kuzuia na kujitayarisha kwa majanga. Malaria inaweka mzigo mkubwa katika mifumo ya afya yenye rasilimali tete na kidogo. Sio tu kwamba kuibuka tena kwa Malaria kutadhoofisha mifumo ya afya, kupunguza uwezo wa nchi katika kutambua na kutibu hali zote za afya kwa ufanisi, lakini pia kungepunguza uwekezaji mwingine katika kuimarisha mfumo wa afya na kudhoofisha ulinzi dhidi ya magonjwa mengine na kusababisha ukosefu mkubwa wa usalama wa afya duniani.

**Kuibuka tena kwa malaria kungeingiza nchi katika umaskini na kusababisha migogoro ya kiuchumi na kuyumba.** Malaria ni ugonjwa wa umaskini ambao umejikita katika nchi zenye kipato cha chini na watu walio katika mazingira magumu. Nchi za Kiafrika, ndizo zilizoathiriwa zaidi na mgogoro wa kifedha unaoendelea. Wanakabiliwa na viwango vya juu vya madeni na hatari za malipo, na wana rasilimali chache toka vyanzo vya ndani kwa sababu ya mapato duni ya ushuru na gharama kubwa za kukopa.

Kuendelea kuwepo idadi kubwa ya visa vya Malaria kunaweka mzigo mkubwa katika uchumi. Ni sababu kuu ya utoro wa wafanyikazi, inaligharimu bara hilo takriban siku nusu bilioni za kazi kila mwaka. Utafiti, ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa hivi karibuni uliofanywa na Taasisi ya Oxford Economics Africa, unaonesha uhusiano wa karibu kati ya viwango vya Malaria na ukuaji wa uchumi na biashara ya kimataifa na uwezekano wa kuona ongezeko la dola bilioni 127 kwa uchumi wa Afrika na dola bilioni 81 za kukuza biashara ya kimataifa ikiwa malengo yatafikiwa ifikapo mwaka 2030.[4]

**Hitimisho – Sote tuna jukumu la kutekeleza.**
Ni lazima nchi zishiriki ipasavyo, zikiimarisha utekelezaji wa afua na kuimarisha usimamizi na uimarishaji wa mifumo.

Mtazamo mzima wa jamii unahitajika, pamoja na kuanzishwa na kutumia mabaraza ya kisekta yenye wadau mbalimbali, mabaraza ya kutokomeza Malaria; pamoja na sekta binafsi imara, vijana, asasi za kiraia, viongozi wa kidini na ushiriki wa viongozi wa kimila.

Ni muhimu kwamba washirika na wadau wote wafanye kazi ili kuhakikisha kwamba GAVI inayokuja - Ushirikiano wa Chanjo na Ukamilishaji wa Mfuko wa Kimataifa unafanikiwa, na kwamba Malaria angalau inaendelea kupokea matumizi kwa sasa katika mgao toka Mfuko wa Dunia. Kwa kuzingatia dhoruba kamili nchi na jumuiya zinakabiliwa nalo, jitihada zote lazima zifanywe; sio tu kudumisha, lakini kuongeza ufadhili na kubadilisha mwelekeo wa nchi kutoka kudorora na kurudi nyuma hadi kudhibiti na kuondoa kabisa janga la kutisha la Malaria.

Umefika wakati ambapo watoto na akina mama vijana wanalidwa kutokana na madhara ya ugonjwa unaoweza kuthibitiwa na kutibika kikamilifu, ambao unaviondolea mustakbali wa vizazi vya siku zijazo na kuzizamisha Jamii katika lindi la umaskini. Malaria si tu ni tishio la maendeleo; bali ni tishio kwa amani na usalama.

---

[1] Cohen et al Malaria Journal volume 11, (2012)
[2] Personal communication, Malaria Atlas Project
[3] WHO, World Malaria Report (2023)
[4] Sarma et al. The economic burden of malaria (2019)